

HABARI KITAIFA

NARCO yataja mikakati kujiendesha kibiashara

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

MKUU wa Kampuni za Ranchi za Taifa (NARCO), Prof. Peter Msoffe, ametaja mikakati itakayosaidia kampuni hiyo kujiendesha kibiashara zaidi ili kutoa gawio kwa serikali.

Prof. Msoffe ameibainisha mikakati hiyo jana baada ya kumaliza kwa kikao cha makabidhiano ya ofisi na aliyekuwa Kaimu Meneja Mkuu wa NARCO, Masele Shilagi, kilichofanyika kwenye ofisi hizo jijini Dodoma.

Akizungumzia mikakati hiyo Prof. Msoffe, alisema ni pamoja na kuifanya kampuni hiyo iwe kitovu cha umahiri wa masuala yote yanayohusu ranchi.

"Katika kuhakikisha hilo linafanikiwa ni lazima kampuni ijipange katika uzalishaji wa nyama ya kutosha iliyo bora, uzalishaji wa mifugo iliyo bora, kutoa mafunzo kwa wataalam na wafugaji, kujiendesha kibiashara na kuweza kupeleka gawio serikalini," alisema.

Alisema ana matarajio makubwa kuwa hayo kutekelezwa kwa kuwa amekuta kampuni ikiwa inaendelea kuimarika na kwa kushirikiana na viongozi na watendaji wa kampuni watatekeleza mikakati hiyo ambayo itawasaidia kutimiza azma ya serikali kwa kampuni hiyo.

Naye, Masele Shilagi, ambaye alikuwa Kaimu Meneja Mkuu wa Kampuni za Ranchi za Taifa, alisema kampuni imekuwa ikiendelea kuimarika kimapato na kujiendesha bila kutumia ruzuku kutoka serikalini. Pia alisema amesimamia mapato na matumizi na kampuni kupata hati safi. "Kampuni imeweza kupima baadhi ya ranchi zake na kushughulikia migogoro iliyokuwapo ikiwemo ya uvamizi wa wananchi kwenye maeneo ya ranchi," alisema.

Aliwashukuru viongozi na watumishi wa NARCO kwa ushirikiano waliompata kipindi cha uongozi wake na kuwaomba waendeleo kutoa ushirikiano kwa Meneja mkuu mpya.

Naye, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Uzalishaji na Masoko, Stephen Michael, alisema kuwa viongozi na watendaji wana wajibu wa kujipanga vizuri ili kuhakikisha malengo na matarajio ya serikali yanatimizwa.

"NARCO inazo fursa nyingi kwenye uzalishaji wa nyama bora, mifugo bora, malisho na utoaji wa elimu kwa wafugaji," alisema.

Alisema katika kuhakikisha fursa zinatumiwa na mapato yanaongezeka kama serikali ilivyopanga, ni lazima uongozi uone namna bora ya kushirikiana na sekta binafsi lengo likiwa ni kuongeza uzalishaji na kuongeza mapato.

Ser

Na Renath DODOMA

TAASISI : hana na RURL, mkoa sekta zilizo mikiwa kw ni serikali zasilimia 35 ambayo in:

Mkuu w Dodoma, alitoa taar mkutano n uliofanyika

Kibweng ingine ni : asilimia sal zenye asili

Hata hiv shi kweny wa zaidi le wa Dodo kuwa siku

Alisema buzi sita : na utoaji l archi, ebu



Ser

Na Said

NARCO, pang, 1 Masauni Udhibiti (PPRA), wa mas Taasisi z gufu na kuisabal

Masa Dodoma, mazung pamoja laika hiy ya kute chini y: